


**Habari kutoka ECHO Afrika Mashariki Jarida #2 Juni - Agosti 2013**

**Yaliyomo katika taarifa hii:**

Mafunzo kwa Mitandao ya Kilimo Hifadhi
Mabadiliko ya Wafanyakazi wa ECHO
Mikakati ya ECHO Afrika Mashariki katika Hifadhi ya Mbegu kwa Wanamtandao
Ziara za Wanafunzi kwenye kituo cha ECHO Afrika Mashariki
Mjadala juu ya mazao yaliyobadilishwa uasilia [GMOs]
Kuna nini katika mtandao wa “internet”?

Pembeni [Sidebars]: Hizi ni picha za wafanyakazi waliojiunga na ECHO hivi karibuni (Robert Obonyo Okumu na Charles Bonaventure - Bonny), Habari, Jinsi ya kujiunga kirahisi na jamii ya ECHO katika mtandao wa intaneti unabofyaECHOcommunity.org

## Salamu kutoka ECHO Afrika Mashariki!

Hapa katika ofisi ya ECHO Arusha hali ya hewa ni joto, na tunaendelea na juhudi zetu za kukuza na kuongeza kilimo hifadhi kwa majirani, ili kuongezea usalama wao wa chakula. Tumeshirikiana na Shamba Darasa katika mafunzo kuhusu kilimo hifadhi:

## Mafunzo kwa Mitandao ya Kilimo Hifadhi

Simon Kutingila ni mmoja wa wakulima mwenye mafanikio makubwa katika kijiji cha Ekenywa, eneo la jirani na ofisi ya ECHO Afrika Mashariki. Alichaguliwa na kijiji chake kama Mhamasishaji wa Kilimo Endelevu, kutokana na bidii yake; Simon aliwahi kufundisha wakulima mbinu nyingi za kilimo hifadhi, kushiriki katika huduma ya ugani, na kushauri wakulima wenzake na hata wataalam wengine juu ya matumizi ya ng'ombe wa maksaiwanapotumika katika kuvuta zana za kilimo hifadhi.

Katika makala ya kwanza ya jarida la ECHO iliyotolewa mwezi wa Aprili 2013, tulieleza kuhusu mafuriko yaliyoleta uharibifu na kiasi kikubwa cha udongo kilichopotea katika mashamba jirani. Tangu wakati huo, wafanyakazi wa ECHO tulishiriki katika kuhamasisha wanavijiji wavijiji kumi vya jirani kuweka mikakati ya kukomesha hali hiyo. Tulishirikiana na maafisa ugani, Flora Kola na Simon Kutingala, kutoa mafunzo kwa viongozi wa vijiji jinsi yakuandaa na kutunzamakontuakatika mashamba yenye mwinuko, kanuni za kilimo cha mseto, na jinsi kilimo hifadhi inachangia katika kutunza udongo na maji shambani. Tulifundisha kilimo hifadhi kwa njia ya jembe la mkono na zana za maksai, kinadharia na kimatendo.Mafunzo haya yaliyoendeshwa kwenye maeneo matatu tofauti, maafisa ugani na viongozi wa vijiji hamsini na sita na wakulima wengine walihudhuria.

Katika mafunzo aliyotoa Simon, maafisa ugani na wataalam wa shirika la ECHO walishangaa na kuzifurahia njiambalimbali za kufundishia alizotumia mkulima huyu kwani yalitumia njia zote za kinadharia na za kivitendo. Washiriki wa semina waliweza kuona na kushika vifaa vya kilimo hifadhi vinavyovutwa na ng'ombe ili kuelewa urahisi ya kilimo hifadhi (ikiwa ni pamoja na chombo cha kuchimba mtaro – Magoye ripper). Watumishi wa ECHO walifundisha juu ya vyombo vya kupandia bila ya kutifua udongo vinavyojulikana kwa lugha ya kigeni kamaLeplanter, jab planter, subsoiler na ripper. Simon ana miaka sita ya uzoefu katika kuendesha shamba darasa, na wakulima wakewalisaidiwa na wataalam kujua jinsi ya kupambana na maswali magumu kama matatizo ya mifugo, magugu, na upatikanaji wa vifaa. Ziara za washiriki katika semina hizi 3 zilifanyika katika wiki iliyofuata ili kubadilishana mawazo na uzoefu wawakulima na kuhimiza umuhimu wa kuiga yale waliyoyaona.
[Maelezo katika picha:] Simon akionyesha jinsi ya kutumia ng'ombe/ Flora akifundisha kilimo hifadhi/ mmomonyoko wa udongo jinsi unavyotokea wakati wa mvua katika sehemu zenye miteremko

**Mabadiliko ya Wafanyakazi wa ECHO**
Katika miezi hii miwili iliyopita Washauri watatu wa ECHO walihitimishavipindi vyao vya kujitolea, nao ni , Amy VanNocker – Arusha-TZ, Vanessa Reed na Ruth Portnoff – Karamoja-Uganda. Badala yao, washauri wawili wapya ambao mmoja ni wa Uganda na mmoja wa Tanzania waliweza kujiunga na timu ya ECHO Afrika Mashariki. Tafadhali tuwashukuru sana Amy, Vanessa na Ruth kwa kazi yao kubwa na nzuri, na tuwakaribisheni Robert OkumuObonyo(Uganda) na Charles Bonaventure (Bonny) (Tanzania)!

Mwezi Julai, wakurugenzi wa mashirika ya mradi wa Pamoja (TOGETHER) walitembelea na kuona kazi ya timu huko Kotido, Karamoja. Waliweza kusema pongezi kwa kazi nzuri na kisha kwaheri kwa Vanessa Reed na Ruth Portnoff, washauri wa ECHO ambao walifanya kazi pamoja na mradi huo kwa mwaka wa kwanza. Katika kipindi chao Karamoja, Vanessa na Ruth walisaidia kuanzisha majaribio ya kilimo hifadhi vijijini na mashuleni, kujenga makontua katika maeneo yenye mimomonyoko,kupanda miti na nyasi nakufundisha jaribio la kukuza miti iliyokatwa katika hifadhi ili kuboresha uoto wa asili(Farmer Managed Natural Regeneration] katika makorongo katika kijiji cha Tepeth. Walianzisha pia mbinu za kuhifadhi maji[hafirs). (Unaweza kuona baadhi ya mambo hayo katika pichahizi: FMNR Kotido, kuangalia ujenzi wa bwawa la maji)

ECHO inawakaribisha sana Ndugu Robert Okumu Obonyo kama Mshauri. Ana shahada ya Kilimo,na uzoefu mzuri wa kilimo endelevu wa miaka 5 katika jamii ya Karamoja na Sudan ya Kusini. Alifanya kazi na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji Deutsche Welthungerhilfe katika ofisi yao ya Moroto. Kinachompa motisha wa kazi ni kubuni njia za kuhifadhi viumbe hai duniani na kupunguza kuenea kwa jangwa kwakueneza mifumo ya uzalishaji wa chakula endelevu kwa gharama nafuu, na kulinda mazingira na afya. Malengo yake makuu katika mwaka wa pili wa ECHO/ PAMOJA ni kuongeza kilimo hifadhi, kukuza FMNR, kuanzisha chanjo yaNdigana Kali (ECF]) na kudhibiti ugonjwa wa Kideri (Newcastle) kwa kutumia chanjo ya matone (I-2) katika

macho.

Agosti ilikuwa mwezi wa kumwaga mfanyakazi mzuri, Amy VanNocker alipomaliza mwaka mmoja wa mazoezi ya kusaidia kuanzisha ofisi ya ECHO Afrika Masharikihapa mjini Arusha. Wakati wa muda wake hapa, Amy alisaidia sana katika kuandaa Kongamano la ECHO Februari 2013, kuratibu usajili wa washiriki, kutunza vifaa, na kufanya mawasiliano na washiriki zaidi ya180. Yeye alifanya kazi ya kuanzisha na kuendeleza bustani za mfano katika ofisi yetu, kuandaa mtandao wa wadau wa kilimo hifadhi katika kaskazini mwa Tanzania, na kuanzisha mkusanyiko wa mbegu za ECHO Afrika Mashariki na maktaba yake.

Tunayo furaha kumkaribisha Ndugu Charles Bonaventure (aitwaye "Bonny"). Kwa muda mrefu amekuwa mshauriwa kujitolea wa ECHO Afrika Mashariki. Bonny aliwahi kufundisha katika chuo cha mboga na matunda HORTI Tengeru akiwa serikalini tangu mwaka 1986 kabla ya kujiunga na World Vision Tanzania mwaka 2004 kama mkufunzi wa kilimo, alikodumu miaka minane katika nyadhifa mbalimbali kama kiongozi wa timu ya Mradi wa Usalama wa Chakula, Afisa wa Sera na Mratibu wa Programu. Kabla ya kujiunga na ECHO, alifanya kazi na Global Service Corps kama Afisa Tathmini. Bonny anatoka mkoa wa Kilimanjaro, ana mke na watoto watatu. Ana shahada mbilikutoka katika vyuo vya Kilimo SUA – Tanzania na cha maendeleo vijijini (Uholanzi). Bonny anajiunga na ECHO akiwa na malengo ya kuendeleza mbinu za kilimo hai, kupunguza njaa, kuboresha hali ya maisha ya wanyonge, na kuongeza ujasiri wa jamii.

**Habari mpya Kituo cha Mbegu**

ECHO iliweza kukodisha chumba kidogo jirani na ofisi ilikitumike kwa hifadhi ya mbegu, baada ya kupata vifaa vinavyohitajika, pamoja na kujenga chumba baridi. ECHO ina mtazamo wa kuiga mfano wa ECHO Asia, kwa kutumia njia ya CoolBOT (http://storeitcold.com/) na kuhifadhi mbegu katika hali isiyo na mfumo wa hewa (vacuum)ili zisiharibike. Hivi karibuni katika Maonyesho wa Kitaifa Tanzania Agricultural Society (Nane Nane) tulipita kukusanya majina ya makampuni ya mbegu ili kufanya mawasiliano mpya na wauzaji wa kikanda na kuandaa orodha yao (database). Hiyo inaweza kusaidia wanachama wa ECHO kujua ni wapi wanaweza kupata mbegu kwa urahisi. Je, na wewe? Unaweza kutusaidia kuboresha “database” yetu? Chanzo chako cha mbegu ni kipi?Utatusaidia ukijaza utafiti i wetu mfupi hapaili kubadilishana uzoefu na wewe.**Ziara za Wanafunzi kwenye kituo cha ECHO Afrika Mashariki**

Tarehe 30 ya mwezi Julai, zaidi ya wanafunzi thelathini wa klabu ya Roots & Shoots kutoka sekondari ya jirani walikuja kutembelea ofisi ya ECHO Afrika Mashariki. Klabu hii inaratibiwa na Jane Goodall Institute na ina mpango wa kuwawezesha vijana na walimu kuwa watunzaji bora wa mazingira. Baada ya kuangalia video fupi kuhusu kilimo hifadhi kwa njia ya Mungu,(Farming God’s Way), wanafunzi walitembelea eneo la maonyesho ya ECHO ili kujifunza kuhusu mboleana mboji, hifadhi ya maji, kilimo cha matuta marefu,, umwagiliaji na mimea yenye lishe bora. Wanafunzi walipenda wazo rahisi la jisi ya kuhifadhi maji (hafir), na walifurahia uzalishaji wa ‘Tropical Lettuce’; walifurahia ziara kiasi kwamba Mwezeshaji aliahidi kuleta kundi jipya la klabu ya wanafunzi kila mwezi! Unaweza kujifunza zaidi kuhusiana na klabu za mazingira Roots& Shoots hapa: http://rootsandshoots.org/

**Mjadala juu ya mazao yaliyobadilishwa uasiliaGMOs): una msimamo gani?**
Kwa ajili ya mapitio ya mitazamo miwili juu ya suala hilo, sisi kama ECHO hatupendekezi, ila mbinu nyingi tunazopendekeza zinamwezesha mkulima kujitegemea, na hazitegemei zana wala pembejeo za nje. Angalie tovuti ya Kilimo Hai Namibia na kuona taarifa yao kuhusu hatari zinazotokana na 'GMOs' na ushauri wao kuhusu umuhimu wa kulinda usalama wa chakula duniani: http://www.noa.org.na. Kisha usome kutoka www.b4fa.orgkwenyekitabu kinachotetea zaidi GMOs kwawataalam wa 'bioscience'; msimamo wao ni kwamba hakuna njia ya kutatua uhaba wa chakula duniani isipokuwa kukuza GMOs. (Unaweza kukisoma kitabu kupitia tovuti yao hapa bila gharama, bofya (http://www.b4fa.org/insights-biosciences-africa/) Mtu mwingine anaelezea vitisho vinavyotokana na matumizi ya mbolea ya chumvi, na anaonyesha njia mbadala; bofya(http://articles.mercola.com/sites/articles/archive/2013/07/02/fertilizer.aspx)

Siku hizi mkulima mdogo anapaswa kufanya nini? ECHO inakaribisha majadiliano, lakini inataka kutoa ukweli ili kukabiliana na uwongo wowote na utetezi ambayo hauna msingi wa ukweli. Kama Rick Burnette wa ECHO anasema, "Mbinu zinazopendekezwa na ECHO kwa ajili ya wakulima wadogo zinalenga katika kumfanya mkulima aweze kujitegemea zaidi. Teknolojia za GMO ni za juu na kwa kawaida, ni za gharama. Zaidi ya hayo, GMOs ni kinyume cha sheria katika nchi nyingi. Tukifuata vigezo vile, si rahisi kwa ECHO kupendekeza GMOs." Hebu, uongeze mawazo yako kuhusu swali hili.

**Kuna mapya katika www.ECHOcommunity.org?**
Ingia katika www.ECHOcommunity.org kusoma ECHO Maelezo ya Mbinu Bora(#3)yanayolenga kusaidia Wafugaji (pastoralists), mwandishi ni Erwin Kinsey bofya:
http://www.echocommunity.org/?page=BPN

Grant Dryden hivi karibuni alilitoa kitabu kuhusu kilimo cha mbogamboga 'kwa Njia ya Mungu'na unaweza kukipata hapa bofya
http://www.farming-gods-way.org/Resources/Farming_Gods_Way_Vegetable_Guide.pdf
Ni bure kukifungua na kina kurasa 30 ukiwa ni pamoja na jinsi ya kutunza bustani za nyumbani namashamba madogo ya mboga. Kinaeleza aina 11 za mazao, ratiba ya kupanda, jinsi ya kuandaa vitalu, matuta ya kukuzia mbogamboga,, mbinu za umwagiliaji maji wa matone, jinsi ya kutengeneza mboji na mengineyo. Unaweza kujiunga na kikundi kimoja katika mtandao wa FGW katika Facebook (Kenya, Uganda, Eastern Cape,Tanzania) na kupata taarifa ya matukio na machapisho kama haya.

Erwin Kinsey alihudhuria na kufurahishwa na mkutano wa hivi karibuni wa'Kilimo Hai katika Afrika Mashariki' uliofanyika Dar es Salaam. Ukifuata tovuti hapo chini, unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu mkutano huo wa thamani, uliyofadhiliwa na IFOAM (Shirikisho la Kimataifa la Kilimo Hai). Upatikanaji wa maonyesho na mihutasari wa mkutano huo unapatikana hapa:
http://www.ifoam.org/en/events/east-africa-organic-conference
http://www.oisat.org/ hii ni tovuti maalumu katika kudhibiti mashirika yasiyotumia kemikali dhidi ya wadudu &magonjwa katika mimea na mifugo
http://www.eprints/-hapo kuna maelezo mingi kuhusu kilimo hai na utafiti wake
http://www.organic-africa.net./training-manual.html-hiki ni kitabu kuhusu kilimo hai katika Afrika -

Mwongozo wa kufundishia.
http://www.organic-services.com/groupcertification.html tovuti hii inaelezea mfumo shirikishi wa kudhibiti makundi ili kupata vyeti
http://www.ifoam.org/en/osea-ii-project tovuti ya mradi OSEA II ambayo imesaidia kujenga kiwango cha kawaida kwa ajili ya vyeti vya kutimiza matakwa wa kilimo hai (organic standard)

Toleo maalum la ECHO liitwaloEDN120 sasa linapatikana katika www.ECHOcommunity.org. Toleo hili linaelezea jinsi ya kuwekamipango ya shamba. Pia msomaji atapata muhtasari wa jinsi ya kilimo hifadhi katika zao la mpunga,mfano ripoti mpya kutokakwa Norman Uphoff akielezea matumizi na kanuni za zao la mpunga 9System of Rice Intensification – SRI0 na mazao mengine.

Mwongozo mpya wa RIPAT unanaelezea hatua kwa hatua jinsi ya kupanga na kutekeleza mipango ya makundi ya maendeleo nambinu mbalimbali za kilimo endelevu. Ni vyema kusoma kwa wale wanaopenda kuboresha usalama wa chakula na mapato ya wakulima wadogo wadogo. Maelezo yanamfaidi mkulima, lakini pia mwalimu, mtafiti na mtunga sera. Kitabu ni muhimu hasa kwa wafanyakazi wa mashirika yasiyo ya kiserikali na mashirika ya maendeleo katika ngazi ya programu za kilimo, na kwa serikali za mitaa kushirikiana na wataalam wa kilimo na maendeleo vijijini: http://www.ripat.org/downloads/

Katika maadhimisho ya miaka yake 30 ya Canada Food Grains Bank (CFGB), walitaja njia tatu kuu muhimu za kupmabana na changamoto za uhaba wa chakula. Walitaja njia tatu ambazo zinazoweza kufuatwa na kuwa na uhakika wa chakula ni pamoja na: kilimo hifadhi – pamoja na ‘agroecology’, utekelezaji wa haki za kibinadamu kwa chakula cha kutosha, na uwazi zaidi katika njia za kutoa misaada ya chakula. Unaweza kunufaika na njiahizo kwa kubofya hapa:: http://foodgrainsbank.ca/fighting_hunger_conference_details.aspx

**Habari zaidi:**
Mwezi uliopita, Tanzania ilipokea marais watatu wa Marekani, wawili waliostafu, katika ziara mbalimbali. Wiki mbili tu zilizopita, serikali ya Tanzania ilisaini mkataba na“Clinton Initiative”wa Maendeleo yenye kusudila kuongeza uzalishaji wa mbegu kutoka tani 30,000 wa sasa hadi tani 60,000 ifikapo mwaka 2015.www.allafrica.com/stories/201308060172.html

Mapema mwezi uliopita, serikali ya Tanzania, kwa kushirikiana na World Vision Tanzania, ilitoa wito kwa wadau kusaidia FMNR (uone hapo juu) katika jitihada za kupambana na ukataji miti. www.allafrica.com/stories/201307020041.html

**Matukio yanayotarajiwa katika miezi ijayo:**
Mkutano wa Afya, Kilimo, Utamaduni - pamoja na Jumuiya ya ECHO Florida, USA
30 Septemba – 4 Oktoba, 2013 inaandaliwa na ECHO USA
Kwa habari zaidi tazama: http://www.echocommunity.org/events/event_details.asp?id=272803

Mkutano: Wa kidigitalikatika matumizi ya Kilimo

Kigali, Rwanda
4-8 Novemba, 2013
Unaandaliwa na CTA -Uholanzi na Wizara ya Kilimo, Rasilimali, na Wanyama - Rwanda
Kwa habari zaidi tazama: http://www.ict4ag.org/en/

Mkutano wa Kilimo Hifadhi bila ya kutifua udongo
N. Drakensburg, Afrika Kusini
3-5 Septemba, 2013
Inaandaliwa na South African No-Till Club
Kwa habari zaidi tazama : http://www.notillclub.com/index.php/conference

**Kujiunga bure na ECHOcommunity.org**

Kama wewe siyo mwanachama, sisi tunapenda kupanua wigo kwa kumkaribisha kila mmoja wenu kuwa mwanachama wa www.ECHOcommunity.org bila gharama yeyote. Baada ya kujiunga na mtandao wetu, unaweza kupata rasilimali nyingi kwa njia ya mtandao yaani “internet”kuhusiana na kilimo hai, pembejeo rahisi na kilimo endelevu. Ni matumaini yetu kwamba unaweza pia kubadilishana maarifa na uzoefu wako katika kuwasiliana na watu ana wadau wengine, kufaidika na machapisho yetu kwa kina, na kupata washirika wengine wenye uwezo wa kutatua matatizo yako au kufahamiana na wenzako wanaofanya kazi katika eneo lako. Karibuni Sana!

Tunakaribisha maoni yako na maswali na unaweza kutuma kwa:

Erwin Kinsey : ekinsey@echonet.org
Amy VanNocker : avannocker@echonet.org